

Abstract

Ukinzani ni dhana ambayo imefasiliwa kama ubishi au upinzani. Ukinzani katika methali za Kiswahili unaweza kufasiliwa kama unyume wa kimaana unaoletwa na methali ambazo ziko katika jazi moja na zinazotoa maana zilizo kinyume. Methali za Kiswahili zina maana na ili maana hiyo ijitokeze kwa namna inayofaa, kila methali inapaswa kutumika katika mazingira yanayooana na maana ya methali mahususi. Methali zina jukumu la kuonya, kusifu, kukashifu, kuelekeza, kuliwaza na kadhalika. Aidha, katika fasihi ya Kiswahili kuna jazi za methali zilizo na maana kinyume. Kwamba, methali moja inakuelekeza huku na nyingine inakupa mwelekeo unaotofautina na ule wa awali. Katika hali kama hii, mtumiaji lugha na mwanajamii kwa jumla anaweza kupatwa na utata wa mwelekeo atakaoufuata. Methali zinapota maana zinazopingana basi utata unaweza kujitokeza haswa ukimsemea nwanajamii methali kisha naye akutajia iliyo na maana kinyume, huenda suluhu ya mnachozungumzia ikakosekana. Hali hii ndiyo ilimsukuma mtafiti akitaka kubainisha namna wanajamii wanavyochukulia kuwepo kwa ubishi katika methali za Kiswahili, ikizingatiwa kwamba methali hizi hutumika kila mara na wanajamii katika mazungumzo, nyimbo na hata katika uandishi.